



**SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU
NA MALI YA AMANA NAM.2
YA MWAKA 2007**

KANUNI ZA HIBA

NA WAKFU

ZA KIISLAMU

2011

**ZANZIBAR
JANUARI, 2011.**

**SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI
YA AMANA NAM.2 YA MWAKA 2007**

**KANUNI ZA HIBA NA WAKFU ZA KIISLAMU,
2011**

YALIYOMO

NAM.	JINA	KANUNI	UK.
1.	Yaliyomo	-	
2.	VIFUNGU VYA UTANGULIZI	-	
3.	Jina fupi na kuanza kutumika	1	
4.	Ufafanuzi	2	
5.	Matumizi	3	
6.	VIFUNGU VYA KIDINI	-	
7.	HIBA	-	
8.	Maana ya Hiba	4	
9.	Kufungamana Hiba na kutimia kwake	5	
10.	Hukumu za Ijabu na Kabuli katika Hiba	6	
11.	Uthibitisho wa Hiba	7	
12.	Vinavyotimiza upokeaji wa Hiba	8	
13.	Kupokea Hiba kwa ajili ya mtoto mdogo	9	
14.	Hiba ya mama au mmoja ya wanandoa kwa mwenziwe vitu na vifaa vya nyumbani	10	
15.	Masharti ya Mtoaji Hiba	11	
16.	Masharti ya anayepewa Hiba	12	
17.	Masharti ya kitu kinachotolewa Hiba	13	
18.	Hiba ya ushirika	14	
19.	Hiba ya sheya, nyaraka za mali na haki za mali	15	
20.	Badali katika Hiba ya Masharti	16	

21.	Hiba ya mgonjwa wa maradhi ya mauti	17	
22.	Kughairi katika Hiba	18	
23.	Sababu zinazokubalika kuvunja Hiba	19	
24.	Vizuizi vya kughairi katika Hiba	20	
25.	Matokeo ya kughairi katika Hiba	21	
26.	Yanayobatilisha Hiba	22	
	Kubeba jukumu pindi kikihiliki kitu kilichotolewa Hiba	23	
27.	WAKFU	-	
28.	Maana ya Wakfu	24	
29.	Tamko la Wakfu	25	
30.	Vigawanyo vya Wakfu	26	
31.	Masharti ya kukubalika Wakfu	27	
32.	Sharti za kutekeleza Wakfu	28	
33.	Vitu vinavyofaa kuwekwa Wakfu	29	
34.	Haki ya Kuweka Masharti	30	
35.	Kushuhudisha Wakfu na kubadilisha matumizi yake au masharti	31	
36.	Kusajiliwa Wakfu wa Mali isiyohamishika	32	
37.	Kuteuliwa msimamizi wa Wakfu na kumbadilisha	33	
38.	Wakfu wa msikiti	34	
39.	Sharti zisizozingatiwa	35	
40.	Ufahamu wa sharti za Wakfu na tafsiri yake	36	
41.	Wakfu uliotegemezwa baada ya kufa	37	
42.	Kubadilisha kitu kilichowekwa Wakfu	38	
43.	Sharti za anayewekwa Wakfu	39	
44.	Sharti za chenye kuwekwa Wakfu	40	
45.	Kuugawanya Wakfu	41	
46.	Kumuengua msimamizi wa Wakfu	42	
47.	Kughairi katika Wakfu wa kusaidia kheri	43	
48.	Kughairi katika Wakfu wa familia	44	
49.	Hali ambazo haifai kughairi katika Wakfu	45	
50.	Kuufunga Wakfu wa familia	46	
51.	Kugaiwa tirka katika hali ya kufunga Wakfu wa familia	47	
52.	TARATIBU ZA USIMAMIZI WA KAMISHENI	-	
53.	Uwekaji wa Wakfu	48	
54.	Amana na aina zake	49	
55.	Uwekaji wa Amana	50	
56.	Kurejeshwa kwa Amana	51	
57.	Ukodishwaji wa Mali ya Wakfu au Amana	52	
58.	Mikataba ya upangaji	53	

59.	Uhalali wa mpangaji	54	
60.	Kifo cha Mpangaji	55	
61.	Wajibu wa Warithi wa Mpangaji	56	
62.	Kukosekana kwa taarifa na ridhaa ya Warithi	57	
63.	Matumizi ya Mali za Wakfu na Amana	58	
64.	Taasisi kupewa kipaumbele	59	
65.	Malipo ya Kodi	60	
66.	Madeni	61	
67.	TARATIBU ZA KUFANYA MATENGENEZO	-	
68.	Matengenezo ya mali ya Wakfu na Amana	62	
69.	Mpangaji kufanya matengenezo	63	
70.	Gharama za matengenezo	64	
71.	Uharibifu unaofanywa na mpangaji	65	
72.	Ukaguzi na ufuatiliaji wa mali za Wakfu na Amana	66	
73.	Uvamizi wa mali za Wakfu na Amana	67	
74.	MAKOSA MBALIMBALI NA ADHABU ZAKE	-	
75.	Makosa na adhabu zake	68	
76.	MENGINEYO	-	
77.	Fomu na nyaraka mbalimbali	69	
78.	Marekebisho	70	
79.	JADUWELI	-	
	1. Fomu ya Utoaji Hiba (gift)	-	
	2. Fomu ya Uwekaji wa Wakfu	-	
	3. Waraka wa Hiba (Kiswahili)	-	
	4. Waraka wa Hiba (Kiingereza)	-	
	5. Waraka wa Wakfu (Kiswahili)	-	
	6. Waraka wa Wakfu (Kiingereza)	-	
	7. Waraka wa Kukabidhiwa Amana ya Mirathi	-	

SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA NAM. 2 YA 2007

KANUNI ZA HIBA NA WAKFU

(Chini ya kifungu cha 67 (1))

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 67 (1) cha Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana ya 2007, Mimi, **ABUBAKAR KHAMIS BAKARY**, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar natunga Kanuni zifuatazo:-

VIFUNGU VYA UTANGULIZI

- Jina fupi na kuanza Kutumika. 1. Kanuni hizi zitajulikana kama ni Kanuni za Hiba na Wakfu za Kiislamu, 2010 na zitaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Waziri.
- Ufafanuzi. 2. Katika kanuni hizi isipokuwa maelezo yakihitaji vyenginevyo:-
- “Badali” Maana yake ni kitu chochote mbadala ya kitu chengine.
- “Bodi” Maana yake ni Bodi ya Uongozi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kama inavyopatikana chini ya kifungu cha 5 cha Sheria.
- “Ijabu” Maana yake ni kauli ya mtu wa kwanza kati ya wanaotaka kufanya mafungamano juu ya kitu fulani.
- “Kabuli” Maana yake ni Kauli ya mtu wa pili kati ya wanaotaka kufanya mafungamano kuhusu kukubali kwake.
- “Kamisheni” Maana yake ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.
- “Kifungu cha Sheria ya Kiislamu” Maana yake ni Aya ya Qurani tukufu au Hadithi ya Mtume (S.A.W).
- “Kuukosa utu” Maana yake ni hali ya kuwa mtoto mdogo au kuwa mgonjwa wa akili.
- “Mahkama” Maana yake ni Mahkama ya Kadhi au Mahakama yenye mamlaka.
- “Mali inayothaminika” Maana yake ni kila mali yenye thamani au maana katika jamii kwa mfano isiwe punje ya mchele au punje ya mchanga.
- “Maradhi ya Mauti” Maana yake ni maradhi ambayo humpata mwanadamu na anadumu nayo hadi anafariki dunia ndani ya mwaka mmoja.

“Mtoto mdogo” Maana yake ni mtoto mdogo asiyekuwa mpambanuzi ambaye bado hajafikia umri wa miaka kumi tokea kuzaliwa kwake.

“Mtoto Mpambanuzi” Maana yake ni mtoto aliyefikia umri wa miaka kumi na zaidi tokea kuzaliwa kwake.

“Mtoto mpungufu” Maana yake ni mtoto ambaye bado hajafikia umri wa kubeba jukumu la jinai na anaingia katika kundi hili mtu aliyekosa utu wake au uliyepungua utu wake.

“Mwenye kuzuiliwa kisheria” Maana yake ni Mtu aliyezuiliwa na Kadhi au Mahakama kufanya matumizi yoyote katika mali yake kutokana na sababu mbali mbali kama vile ufujaji wa mali, ubadhirifu, kukopa sana, kudaiwa madeni sana n.k.

“Sheria” Maana yake ni Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Nam.2 ya 2007 pamoja na marekebisho yake.

“Taasisi za misaada au elimu au njia za kheri” Maana yake ni kila Jumuiya au sehemu inayotoa huduma za jamii kama vile Msikiti, Madrasa, Chuo, Hospitali, skuli n.k.

“Utu kamili au aliyekamilika utu wake” Maana yake ni kila mtu madhali kanuni hizi hazijaeleza vyenginevyo.

“Waziri” Maana yake ni Waziri anayesimamia Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar.

Matumizi. 3. Bila ya kuathiri matakwa ya Sheria, Kamisheni katika kutekeleza majukumu na kazi zake itazingatia misingi ya Kanuni hizi.

VIFUNGU VYA KIDINI

HIBA (GIFT)

Maana ya Hiba. 4. (1) – Hiba ni kumilikisha mali au haki ya kimali kwa mtu mwengine wakati wa uhai wa mmiliki wa awali bila ya badali au malipo yeyote.

(2) – Inaruhusiwa kutoa Hiba kwa badali kama vile mtoaji Hiba kushartisha kwa mtu aliyempa hiba kutoa badali ya kimali au kufanya kazi fulani.

Kufungamana Hiba na kutimia kwake. 5. Hiba inafungamana kwa Ijabu (Offer) na kabuli (acceptance) na inakamilika kwa kupokea Hiba hiyo.

Hukumu za Ijabu na Kabuli katika Hiba. 6. (1) – Ijabu ya Hiba inakuwa sahihi kwa kila namna inayojulisha kumilikisha mali bure, sawa sawa iwe kwa kutamka, kuandika au kwa ishara zenye kufahamika.

(2)- Inafungamana Hiba kwa kupeana.

Uthibitisho Wa
Hiba.

7. (1) – Hiba ya matamshi inalazimu kuthibitishwa kwa uchache na mashahidi wawili wanaume watu wazima au mwanamme mmoja mtu mzima na wanawake wawili watu wazima.

(2) – Hiba ya maandishi inalazimu kuthibitishwa kwa hati maalumu ya Waraka wa Hiba uliosajiliwa rasmi.

(3) – Hiba ya ishara inalazimu kuthibitishwa na mtaalamu wa alama za ishara mwenye kutambulikana.

Vinavyotimiza
Upokeaji wa Hiba.

8. (1) - Upokeaji wa Hiba unasimama nafasi ya Kabuli ya matamshi.

(2) - Upokeaji wa Hiba upo wa hakika na upo wa kihukumu kama ifuatavyo:-

(a) Kupokea kwa hakika kwa mali isiyohamishika ni kama kukaa kwenye nyumba iliyotolewa Hiba, au kuikodisha au kuitawalia na kuitumia kwa namna yeyote inayojulisha kuimiliki.

(b) Kupokea kwa hakika kwa mali inayohamishika kunatimia kwa njia ya kukabidhiwa mali hiyo.

(c) Kupokea kwa hukumu kwa mali isiyohamishika kunatimia kwa kujitoa (ejectment) kunakopelekea utawala bila ya kizuizi, na kwa kusajili katika Idara inayohusika na kwa kupokea funguo za nyumba au kitu chenginecho.

(3) - Hiba inatimia kwa ljabu pekee ikiwa kitu kinachotolewa Hiba kimo mikononi mwa anayepewa Hiba.

Kupokea Hiba kwa
ajili ya mtoto mdogo.

9. (1) - Ikiwa mtoaji Hiba kwa mtoto mdogo (minor) si walii wake wala si wasii wake wala si mlezi wake, basi Hiba itatimia kwa kupokea yeyote kati ya hao (walii,wasii au mlezi).

(2) - Hiba kwa mtoto mdogo itatimia kwa ljabu pekee ikiwa mtoaji Hiba ni walii wake au wasii wake au mlezi wake.

(3) - Inaruhusiwa kwa mtoto mdogo mpambanuzi kukubali Hiba na kuipokea Hata kama anaye walii.

Hiba ya mama au
mmoja ya wanandoa
Kwa mwenziwe vitu na
Vifaa vya nyumbani.

10. - Inasihhi na kukubalika Hiba ya mama kwa mtoto wake mdogo au Hiba ya mmoja wapo kati ya mume na mke kwa mwenzake kitu au kifaa au pambo kati ya vitu vya nyumbani, au mnyama, kipando n.k, pindi akishuhudisha Hiba hiyo hata kama hakunyanyua mkono wake kwa mali anayoitolea Hiba.

Masharti ya mtoaji Hiba. 11. – Ili Hiba iwe sahihi ni lazima mtoaji Hiba awe na sifa zifuatazo:-

- (a) – Awe ni mtu mwenye utu kamili, baleghe, mwenye akili timamu, mwenye kufanya kwa hiari yake, asiwe mwenye kuzuliwa na Sheria ya Kiislamu au sheria yoyote na wala asiwe mgonjwa wa maradhi ya mauti.
- (b) – Awe ni mmiliki halali wa kitu anachokitoa Hiba.

Masharti ya Anayepewa Hiba. 12. – Ili Hiba iwe sahihi ni lazima kwa mtu anayepewa Hiba awepo, hivyo haitokuwa sahihi kutolewa Hiba kwa mtu asiyekuwepo ulimwenguni wala kwa mimba.

Masharti ya kitu Kinachotolewa Hiba. 13. – Ili Hiba iwe sahihi ni lazima kwa kitu kinachotolewa Hiba kiwe:

- (a) – Ni mali inayothaminika.
- (b) – Kipo wakati wa kutolewa Hiba.
- (c) – Ni chenye kumilikiwa na mtoaji Hiba.
- (d) – Ni chenye kujulikana wazi wazi.

Hiba ya Ushirika. 14. - Inaruhusiwa kutoa Hiba ya pamoja (intercommon) sawa sawa ni ya kuachia (absolute) au imeshikamana na mtu mwengine, mshikamano wa kugandana au wa ujirani.

Hiba ya Sheya, nyaraka za mali na haki za mali. 15. - Inaruhusiwa kutoa Hiba sheya, nyaraka za fedha (securities,stocks) na haki nyenginezo za kimali.

Badali katika Hiba ya masharti. 16.(1)- Bila ya kuathiri maelezo ya para ya (2) ya Kanuni ya 4, inapasa badali (instead of something) iwe ni kitu chenye kujulikana katika Hiba ya masharti, vyenginevyo kila upande (party) una haki ya kuvunja mafungamano ya Hiba (revocation of the agreement) hata kama tayari kitu kilichotolewa Hiba kimeshapokelewa, madhali hawakuwafikiana juu ya badali fulani kabla ya kuvunja makubaliano hayo.

(2) – Kama kikifa au kuharibika kitu kilichotolewa Hiba katika Hiba ya masharti au tayari amekwishakutumia mtu aliyepewa Hiba, kabla ya kuvunjika mafungamano ya Hiba, itamlazimu kurejesha thamani yake kwa thamani ya siku aliyopokea Hiba hiyo.

Hiba ya mgonjwa wa Maradhi ya mauti. 17. Zitatumika katika Hiba ya mgonjwa wa maradhi ya mauti hukumu za Wasia.

Kughairi katika Hiba. 18. – Inakubalika kwa mtu aliyetoa Hiba kughairi (ademption) katika Hiba yake:-

- (a) – Kabla ya kupokea, bila ya ridhaa ya aliyepewa Hiba.
- (b) – Baada ya kupokea, kwa ridhaa ya aliyepewa Hiba, na kama hakuridhia basi inaruhusiwa kwa mtu aliyetoa Hiba kudai

kuvunja mafungamano ya Hiba kwa sababu zenye kukubalika madhali hakuna kizuizi chochote cha kughairi.

Sababu zinazo- 19. Bila ya kuathiri maelezo ya Kanuni ya 20 ya Kanuni hizi, zifuatazo zitakubalika kuwa Kubalika kuvunja Hiba. ni sababu za kuvunja mafungamano ya Hiba na ni sababu za kughairi katika Hiba :-

- (a) – Kushindwa kujihudumia mtoaji Hiba au kushindwa kumhudumia mtu anayemtegemea.
- (b) – Mtoaji Hiba ambaye alikuwa hana mtoto akaruzukiwa baada ya kutoa Hiba mtoto ambaye ameendelea kuwa hai hadi tarehe ya kughairi, au anaye mtoto aliyemdhania kafa wakati alipotoa Hiba kumbe bado angali hai.
- (c) - Kuvunja wajibu wake mtu aliyepewa Hiba, wajibu uliolazimishwa kwenye mafungamano ya Hiba bila ya sababu zinazokubalika, au akavunja wajibu wake kwa mtoaji Hiba au mmoja wa jamaa zake, kiasi kwamba uvunjaji huu unahesabika ni kukiuka makubaliano kwa upande wake.

Vizuizi vya kughairi 20. - Vifuatavyo vitahesabiwa kuwa ni vizuizi vya kughairi katika Hiba:-
Katika Hiba.

- (a) – Hiba kuwa inatokana na mmoja kati ya wanandoa wawili kwa mwenzake au maharimu wake (prohibited degrees of marriage) madhali haujajitokeza upendeleo kati yao bila ya sababu za kisheria (justification).
- (b) - Kukitumia chote kitu kilichotolewa Hiba, mtu aliyepewa Hiba, matumizi yanayohamisha umiliki (ownership), ikiwa amekitumia sehemu tu na siyo chote inafaa kughairi kwa kile kilichobaki.
- (c) - Kukiongeza kitu kilichotolewa Hiba nyongeza iliyoshikamana nacho au kukibadilisha muundo wake kwa ziada inayobadili jina lake.
- (d) - Kufariki mmoja ya wanaopeana Hiba baada ya kuipokea Hiba hiyo.
- (e) - Kuharibika au kuhiliki chote, kitu kilichotolewa Hiba mikononi mwa mtu aliyepewa Hiba, kama ikiwa kitahiliki sehemu tu na siyo chote basi inafaa kughairi kwa kilichobaki.
- (f) - Ikiwa Hiba ni ya badali.
- (g) – Hiba kuwa ni ya taasisi ya kheri, au mdai kutoa Hiba deni kwa anayemdai.

Matokeo ya kughairi katika Hiba.

21. (1) - Kughairi katika Hiba, iwe kwa ridhaa au kwa hukumu ya Mahkama kunahesabika ni kubatilisha matokeo ya mafungamano ya Hiba.
- (2) - Hatorudisha mtu aliyepewa Hiba manufaa yeyote aliyoyapata kwenye kitu alichopewa Hiba, isipokuwa tokea siku ya tarehe ya kughairi kwa ridhaa au siku ya tarehe ya hukumu ya Mahkama.
- (3) - Inakubalika kwa mtu aliyepewa Hiba kudai gharama za lazima alizozitumia kwenye kitu alichopewa Hiba, ama gharama zisizokuwa za lazima hatorejeshewa isipokuwa zikizidi thamani ya kitu kilichotolewa Hiba.

Yanayobatilisha Hiba.

22. - Hiba inabatilika kutokana na lolote kati ya mambo yafuatayo:-
- (a) – kukosekana nguzo au sharti yeyote kati ya sharti zilizotajwa ndani ya Kanuni hizi.
- (b) - Kuchelewa kukichukua kitu kilichotolewa Hiba hadi mtoaji Hiba akazidiwa na deni au madeni, ijapokuwa yamekuja baada ya kutoa Hiba.

Kubeba jukumu (Responsibility) Pindi kikihiliki kitu Kilichotolewa Hiba.

23. (1) - Akidai mtoaji Hiba arejeshewe kitu alichokitowa Hiba bila ya ridhaa au bila ya hukumu ya Mahkama, atabeba jukumu (responsibility) yeye wakati wa kuhiliki kitu hicho kwa sababu yeyote itakayokuwa.
- (2) - Ikitoka hukumu ya Mahkama ya kughairi katika Hiba na kitu kilichotolewa Hiba kikawa kimehiliki mikononi mwa mtu aliyepewa Hiba baada ya kumuonya akikabidhi kitu hicho, basi atabeba jukumu yeye kwa uharibifu wowote uliotokea na kwa sababu yeyote itakayokuwa.

WAKFU

Maana ya Wakfu.

24. - Wakfu ni kuizuia mali kwenye hukmu ya M/Mungu na kutolea sadaka manufaa yake katika hali au mali.

Tamko la Wakfu.

25. - Panashartishwa katika uwekaji wakfu, tamko la Wakfu:-
- (a) – Liwe timilifu lenye mafanikio (completed and achieved).
- (b) – Liwe la daima.
- (c) – lisikutane na sharti lolote lenye kupingana na hukmu za Wakfu.

Vigawanyo vya Wakfu.

26. - Wakfu unagawanyika vigawanyo vitatu kama ifuatavyo:-
- (a) – Wakfu wa kusaidia kheri (charitable Wakf) ni Wakfu ambao unatoa manufaa yake tokea awali kwenye taasisi za kutoa huduma za kheri (charitable institutions).

(b) – Wakfu wa familia ni Wakfu unaotoa manufaa yake tokea awali ama kwa mtoaji wakfu mwenyewe au mtu maalumu au mwengine aliyesainishwa kwa lengo hilo.

(c) – Wakfu mshirika ambao ndio ule unaokhusisha (specify) kwa pamoja manufaa yake kwa familia na kwa taasisi za kutoa huduma za kheri.

Masharti ya kukubalika Wakfu. 27.

- Ili wakfu ukubalike ni lazima mtoaji wakfu awe:-

(a) – Balebhe, mwenye akili timamu na ni mwenye sifa za kutoa msaada.

(b) – Hajazuiliwa kufanya matumizi kutokana na ama kufanya matumizi mabaya au kusahausahau.

Sharti za kutekeleza Wakfu. 28.

- Ili wakfu utekelezwe ni lazima mtoaji wakfu asiwe:-

(a) – Amezuiliwa matumizi kisheria kwa sababu ya madeni.

(b) – Mgonjwa wa maradhi ya mauti.

Vitu vinavyofaa Kuwekwa Wakfu. 29.

(1) – Inakubalika kuweka Wakfu kila mali yenye kuthaminika sawa sawa ni mali isiyohamishika au inayohamishika, na inakubalika kuweka wakfu kila kinachowekeka wakfu kidesturi ikiwemo fedha (cash wakfu).

(2) – Ni wajibu kwa kiasi au kiwango kinachowekeka wakfu kwenye mali isiyohamishika kiwe kimetenganishwa au kinajitegemea wenyewe na si cha pamoja ila msikiti au makaburi.

Haki ya kuweka masharti. 30.

(1) – Inaruhusiwa kwa muwekaji wakfu yeye mwenyewe au mtu mwengine kuweka masharti juu ya haki ya kutoa au kuzuia, kuingiza au kutoa, kuzidisha au kupunguza, kubadilisha au kubadilishiwa na haki ya kufadhilisha au kukhusisha, inaruhusiwa kwa yeye mwenyewe au kwa huyo mtu mwengine kuitumia haki hiyo kwa utaratibu uliotajwa wakati wa kushuhudisha wakfu.

(2) – Inaruhusiwa kwa muwekaji wakfu kubadilisha matumizi ya wakfu na sharti zake hata kama alijizuilia hayo tokea mwanzo.

Kushuhudisha Wakfu na kubadilisha matumizi yake au masharti. 31.

Ubadilishaji wa matumizi ya Wakfu au masharti yake unakamilika kwa ushuhuda rasmi mbele ya Mahkama yenye mamlaka kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Kusajiliwa Wakfu wa mali isiyohamishika. 32.

- Ikiwa uwekaji wakfu ni wa mali isiyohamishika basi italazimu kusajiliwa katika taasisi iliyotajwa na sheria maalumu ili kutekeleza matakwa ya sheria hiyo.

Kuteuliwa msimamizi 33.

- Inaruhusiwa kwa muwekaji wakfu kumteuwa muangalizi na msimamizi

- wa wakfu na kumbadilisha. wa wakfu kama ambavyo inafaa kumbadilisha hata kama hakujiwekea sharti hilo.
- Wakfu wa msikiti. 34. (1) – Haifai na wala hairuhusiwi kuubadilisha wakfu wa msikiti wala waliowekewa wakfu huo.
(2) – Hayatotumika maelezo ya Kanuni ya 31 kwa wakfu wa msikiti itakapokuwa wakfu huo upo na umeshaanza kutumika kiibada.
- Sharti zisizozingatiwa. 35. (1) – Halitozingatiwa sharti lolote linalopingana na sheria za kiislamu, au linalolazimisha kupotea, au kukosekana maslahi ya waliowekewa wakfu huo.
(2) – Wakfu wowote uliokutanishwa na sharti lisilo sahihi, wakfu huo utakuwa sahihi na litakuwa batili sharti hilo.
- Ufahamu wa sharti za wakfu na tafsiri yake. 36. (1) – Sharti la muwekaji wakfu linakuwa sawa na kifungu cha sheria ya kiislamu katika ufahamu na utambulisho (ujulisho) wake.
(2) – Inaruhusiwa kwa Mahkama wakati wa kuombwa, kuvitafsiri vifungu na sharti za muwekaji wakfu kwa namna inayowafikiana na ujulisho wake.
- Wakfu uliotegemezwa baada ya kufa. 37. - Zitatumika hukmu za vifungu vya wasia katika wakfu uliotegemezwa baada ya kufa.
- Kubadilisha kitu kilichowekwa wakfu. 38. - Kiasili Wakfu haubadilishwi, lakini Ili kupatikane usahihi wa kubadilisha au kutaka kubadilishwa kitu kilichowekwa wakfu ni lazima:-
(a) – Kusiwe na tofauti kubwa baina ya thamani ya wakfu na kinachobadilishwa kwa wakfu.
(b) – Kusiwe na tuhuma yoyote katika kubadilishana.
(c) –Wakfu na kile kinachotaka kubadilishana na wakfu viwe ni vyenye kulingana pindi muwekaji wakfu akiweka sharti hilo.
(d)– Isiwe ile kutaka kubadilishiwa ni kuuza kitu kilichowekwa wakfu kwa thamani ambayo ni deni la mnunuzi kwa mtu anayetaka kubadilisha.
- Sharti za anayekewa wakfu. 39. - Ili wakfu uwe sahihi ni lazima mwenye kuwekewa wakfu awe: -
(a) – Ukaribu wake uko kwenye hukmu ya uislamu.
(b) – Ameainishwa kwa jina au wasifu.
(c) – Yupo, ikiwa ameinishwa kwa jina.
- Sharti za chenye 40.- Ili wakfu uwe sahihi ni lazima kitu kinachowekwa wakfu kiwe :-

kuwekwa wakfu.

(a) – Kinajulikana waziwazi bila ya shaka wakati wa kuwekwa wakfu.

(b) – Kinamilikiwa kwa ukamilifu na muwekaji wakfu na wala hapana sharti la khiari ndani yake wakati wa kuweka wakfu.

Kuugawanya wakfu.

41. (1) – Haifai kuugawa wakfu kwa ajili ya kumiliki kati ya waliowekewa wakfu, isipokuwa inaruhusiwa kukubaliana kwa maridhiano.

(2) – Ikiwa kitu kilichowekwa wakfu ni hisa ya pamoja ya ushirika kati ya muwekaji wakfu na mmiliki mwengine, au ni ushirika kati ya wawekaji wakfu wawili, inaruhusiwa kukigawa kati ya muwekaji wakfu na mshirika mmiliki mwengine au kati ya wawekaji wakfu wawili baada ya kupata idhini ya Mahkama yenye mamlaka.

Kumuengua

42. – Inaruhusiwa kwa Mahkama kutokana na ombi la wahusika kumuengua msimamizi wa wakfu au muangalizi wa wakfu hata kama yeye ndiye muwekaji wakfu au ni mtu aliyeteuliwa na yeye ikithibiti khiyana yake au kikiwepo kizuizi cha kisheria cha usimamizi wake, kama inavyoruhusika kwa Mahkama kumuongeza mtu mwengine ikiwa aliyepo atashindwa kusimamia wajibu wake peke yake, na ikiwa muangalizi au msimamizi wa wakfu ameteuliwa na Mahkama basi inaruhusiwa kumuengua ikiwa na sababu za kufanya hivyo, kama inavyoruhusiwa kumuweka mtu mwengine kwa muda hadi itakapomalizwa kabisa kabisa kesi ya kuenguliwa kwake.

Kughairi katika wakfu wa kusaidia kheri.

43.- Haifai na wala hairuhusiwi kwa muwekaji wakfu kughairi katika wakfu wa kusaidia kheri.

Kughairi katika wakfu wa familia.

44. Inaruhusika kwa muwekaji wakfu kughairi katika wakfu wa familia kwa ushahidi wa kisheria katika Mahkama yenye mamlaka.

Hali ambazo hazifai kughairi katika wakfu.

45 – Haifai wala hairuhusiwi kughairi katika wakfu kwa yoyote kati ya hali zifuatazo:-

(a) –Kufa muwekaji wakfu, hawana haki warithi wake kughairi katika wakfu waliourithi ikiwa ulitimia sharti zake.

(b)– Kupokea kitu kilichowekwa wakfu au pato lake watu waliowekewa wakfu wote au baadhi yao au wakala wao katika uhai wa muwekaji wakfu, kwa maelezo kwamba haitohesabika kwamba ni kizuizi cha kughairi katika wakfu muwekaji wakfu kumiliki yeye mwenyewe katika uhai wake kitu chenyewe au pato lake.

(c) - Kutolewa hukumu na Mahkama ya kulazimisha kuweka wakfu ili kutatua mgogoro uliopo ndani yake.

Kuufunga wakfu wa familia.

46.- Inaruhusiwa kwa Mahkama kuufunga wakfu wa familia kwa yoyote kati ya hali zifuatazo:-

(a) – Kushindikana kunufaika na wakfu huo kwa sababu ya idadi kubwa ya

wanaostahiki.

- (b) – Faida ndogo inayopatikana kutokana na pato lake kwa sura ya kwamba halipatikani lengo la muwekaji wakfu la kuweka wakfu.
- (c) – Kuwa katika hali ya hatari, kubomoka kitu kilichowekwa wakfu na ikashindikana kutengenezwa kwa sababu ya kutokuwepo hali ya kusaidiana au kuwepo ugomvi kati ya wanaostahiki.
- (d) – Muwekaji wakfu kuwazuia baadhi ya warithi wake kufaidika na pato la wakfu, au kuwapendelea baadhi yao kwa kiasi kinachokubalika.

Kugaiwa tirka katika hali ya kufunga wakfu wa familia. 47. - Katika hali ya kuufunga wakfu wa familia, kitu kilichowekwa wakfu kita-hesabika ni tirka na kitagaiwa kwa mujibu wa mafungu ya kisheria ya warithi, ama kwa wale waliowekewa wakfu patachukuliwa hukumu za wasia.

TARATIBU ZA USIMAMIZI WA KAMISHENI

Uwekaji wa Wakfu. 48. (1) – Uwekaji Wakfu wa mali yoyote unatakiwa kufuata matakwa yote ya Sheria ya Kiislamu, Sheria ya Kamisheni na Kanuni hizi.

- (2) – Bila ya kuathiri chochote hakuna Wakfu utakaozingatiwa ila kwa hati rasmi ya Waraka wa Wakfu uliotolewa na Kamisheni.
- (3) – Waraka wa Wakfu utatayarishwa baada ya Muwekaji Wakfu kujaza fomu maalumu ya uwekaji Wakfu.
- (4) – Kabla ya uwekaji wa Wakfu, Muwekaji Wakfu atalazimika kuthibitisha kwa vielelezo juu ya umiliki wake wa mali anayoiwekea Wakfu.
- (5) – Pale ambapo Muwekaji Wakfu amefariki dunia kabla ya kutayarisha Waraka wa Wakfu, Kamisheni itakamilisha Wakfu huo kwa kutoa Waraka wa Wakfu kwa niaba yake.

Amana na Aina zake. 49. Kutakuwa na amana za aina nne kama zifuatazo:-

- (a) – Amana zinazotoka Serikalini.
- (b) – Amana zinazotoka kwenye asili ya mali ya urithi.
- (c) – Amana zinazotoka kwa watu binafsi.
- (d) – Amana za Baitul-Mali na taasisi za dini ya kiislamu.

Uwekaji wa Amana. 50 (1) Uwekaji wa amana wa mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika utakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) – Serikali kukabidhi na kuiweka mali yoyote chini ya usimamizi na uangalizi wa Kamisheni kwa maandishi.

- (b) - Warithi kukabidhi na kuweka chini ya usimamizi na uangalizi wa Kamisheni mali ya marehemu kwa hatua ya kusubiri urithishaji.
 - (c) - Kamisheni kukabidhiwa na kuwekwa chini ya usimamizi na uangalizi wake mali ya amana baada ya kufungwa jalada la urithi au hisabu ya tirka.
 - (d) – Mtu binafsi kwa hiari yake au kwa amri ya Mahkama kuiweka mali yake chini ya usimamizi na uangalizi wa Kamisheni.
 - (e) - Mali zote za tirka ya marehemu muislamu zilizokosa warithi halali kukabidhiwa Kamisheni kwa ajili ya usimamizi na uangalizi wa mali hizo.
 - (f) – Mali za taasisi ama mashirika ya kidini ya kiislamu kukabidhiwa na kuwekwa chini ya usimamizi na uangalizi wa Kamisheni, sawa sawa katika hali ya kawaida au wakati wa dharura.
 - (g) - Kamisheni kuchukuwa udhibiti wa mali za taasisi ama mashirika ya kidini ya kiislamu pale itakaporipotiwa kukosekana msimamizi au vyenginevyo katika hali ya kawaida au hali ya dharura.
- (2) – Kadri inavyowezekana, Kamisheni itakabidhiwa mali yoyote isiyohamishika pamoja na Waraka wa mali hiyo au ithibati nyengineyo.
- (3) - Mara baada ya kuzipokea mali za amana, Kamisheni itazisajili na kutoa hati ya usajili wa amana.

Kurejeshwa 51(1) Bila ya kuathiri matakwa ya Sheria, amana yoyote inaweza kurejeshwa kwa
Kwa amana. mwenyewe kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

- (a) – Muhusika wa mali kuandika ombi la kurejeshwa amana yake kwa Katibu Mtendaji.
 - (b) - Kuthibitisha kwa vielelezo hadi Katibu Mtendaji aridhike kuhusu muhusika, mali anayoomba kurejeshwa, umri wa utu kamili ikiwa sababu ya amana hiyo inatokana na mirathi.
 - (c) - Kujifunga kwa maandishi na kwa watu wazima wawili wa kwenye familia ya muombaji kwamba mali atakayokabidhiwa itawanufaisha wote wanaostahiki, iwapo mmoja au zaidi ya mmoja bado hajakamilisha utu wake kwa mujibu wa Kanuni hizi.
- (2) – Ikiwa Katibu Mtendaji ataridhika na kukubaliana na maombi ya kurejeshwa amana kwa mwenyewe, atairudisha na kuikabidhi amana hiyo kwa maandishi.
- (3) – Wakati wa kurejeshwa amana iliyotokana na kufungwa kwa tirka, Katibu Mtendaji atatoa Waraka wa Urithi au Waraka wa Kukabidhiwa Amana na kumkabidhi muhusika.

- (4) - Kamisheni ikitoa Waraka wa Urithi kwa mujibu wa para 1(c) ya Kanuni hii, itakuwa kuanzia hapo ni kujivua jukumu la amana kwa yeyote asiyekamilisha utu wake.

Ukodishwaji wa 52. Ili ukodishwaji wa mali yoyote ya wakfu au amana uwe halali, ni lazima ufuatae
Mali ya wakfu Au Amana. taratibu zifuatazo:-

- (a) – Muombaji atume kwa Katibu Mtendaji barua ya maombi ya ukodishwaji kwa mali inayohusika ili atoe ridhaa yake ya kukubali au kukataa.
- (b) – Ikiwa maombi yamekubaliwa, muombaji atajibiwa kwa njia yoyote ile, iwe ya maandishi, simu au vyenginevyo na kutakiwa kufika Kamisheni kujaza Mkataba wa Upangaji au Ukodishwaji.
- (c) – Muombaji atajaza mkataba wa upangishaji au ukodishwaji baada ya kuusoma au kusomewa na kuufahamu vyema.
- (d) – Mpangaji kuweka saini yake ndani ya mkataba wa upangishaji ni ushahidi tosha kwamba aliusoma au kusomewa na kuufahamu vyema mkataba huo.
- (e) - Ukodishwaji wa mashamba au vikataa mbali na matakwa ya Kanuni hii, unaweza kufauata taratibu nyengine kama atakavyoona inafaa Katibu Mtendaji.
- (f) – Katika Ukodishaji wa mashamba au vikataa, Katibu Mtendaji anaweza kumuidhinisha mtu yeyote kufanya jambo lolote litakalopelekea ufanikishaji wa ukodishaji huo.

Mikataba ya 53 (1) -Kutakuwa na Mkataba wa Upangaji wa muda mfupi na Mkataba wa Upangaji wa muda mrefu Kamisheni.
Upangaji.

- (2) -Mkataba wa muda mfupi ni mkataba wowote wa upangaji unaofungwa na Kamisheni usiozidi kipindi chake mwaka mmoja.
- (3) - Mkataba wa muda mrefu ni mkataba wowote wa upangaji unaofungwa na Kamisheni unaozidi kipindi chake mwaka mmoja na ambao kwa vyovyote ni lazima uidhinishwe na Bodi na kamwe hautazidi miaka mitano.
- (4) – Mikataba yote ya Kamisheni ni lazima iandaliwe na Mwanasheria katika afisi za Kamisheni.
- (5) – Kwa kuondoa shaka inaelezwa wazi kwamba hakuna upangaji wala upangishaji bila ya mkataba.
- (6) – Kadri inavyomkinika, mkataba wowote utaandaliwa nakala mbili za asili, moja ikiwa ni ya Kamisheni na ya pili ni ya mpangaji.

- (7) – Mpangaji atatakiwa wakati wa kujaza mkataba kuwa na mashahidi wake wawili ambao watasaini mkataba huo.
- (8) – Afisa ama mtumishi yeyote wa Kamisheni hatofaa kuwa shahidi wa mpangaji yeyote, na badala yake atabeba sifa ya ushahidi wa Katibu Mtendaji.
- (9) – Kwa vyovyote itakavyokuwa, mkataba wa upangaji utakuwa na saina saba kama ifuatavyo:-
- (a) – Saina ya Mwanasheria aliyeuandaa mkataba huo.
 - (b) – Saina ya mpangaji.
 - (c) – Saina za mashahidi wawili wa mpangaji.
 - (d) – Saina za mashahidi wawili wa Katibu Mtendaji.
 - (e) – Saina ya Katibu Mtendaji.
- (10) – Mkataba wowote ni lazima uwe na muhuri rasmi (common seal) wa Kamisheni na ubandikwe Stempu kama inavyotakiwa na Sheria ya Ushuru wa Stempu.

Uhalali wa 54 (1) –Mpangaji atahesabiwa kuwa ni mpangaji halali ikiwa atatimiza vigezo vifuatavyo:-
Mpangaji.

- (a) – Awe na mkataba halali wa upangaji unaofanya kazi kwa wakati uliopo.
- (b) – Atekeleze maagizo ya vifungu vyote vinavyomuhusu kwa upande wake katika mkataba wake.
- (c) – Aache makatazo yote yaliyomo yaliyomo katika mkataba wake.

(2) – Miongoni mwa maagizo na makatazo ya Kamisheni kwenye mkataba wowote wa upangaji ni:-

- (a) – Kulipa kodi kikawaida kwa njia ya kitangulizi kabla ya kutumia mali husika.
- (b) - Kuitumia mpangaji mwenyewe mali aliyokodi au ikiwa vyenginevyo basi ni kwa ruhusa ya Kamisheni.
- (c) – Kuacha na kujiepusha mbali na mambo yote au vitendo vinavyokwenda kinyume na Uislamu vikiwemo uuzaji wa ulevi, vinyago, zinaa na kama hayo.
